ARUSHA TECHNICAL COLLEGE
STUDENT'S ORGANISATION OF ARUSHA TECHNICAL COLLEGE
(SOATECO)
P.O BOX 296, ARUSHA, TANZANIA
Email: soatecogallery@gmail.com Instagram: officialsoateco: Soateco_

## PRIME MINISTER'S OFFICE

Mheshimiwa Raisi, Serikali, ya wanafunzi SOATECO 2024/2025.

Mheshimiwa, Makamu wa Raisi, Serikali, ya wanafunzi SOATECO 2024/2025

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali, ya wanafunzi SOATECO 2024/2025

Mheshimiwa Katibu Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali, ya wanafunzi SOATECO 2024/2025

Waheshimiwa Mawaziri mliopo, Manaibu waziri Mliopo, Makatibu wa Wizara zote mliopo, Waheshimiwa wageni waalikwa wote mliopo katika ukubumbi huu,

Amani iwe kwenu

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Soateco Mpya, HARUNA

HARUNA, Soateco mpya.

## RIPOTI YA WIZARA YA ELIMU 2024/2025

UTANGULIZI:

Wizara ya Elimu ni moja kati ya wizara zinazofanya kazi katika serikali ya wanafunzi SOATECO. Wizara hii ina jukumu la kuhakikisha inafatilia kwa ukaribu masuala na maslahi yote ya kitaaluma kwa wanafunzi wote. Wizara ya Elimu inaundwa na jumla ya viongozi wane kama ifuatavyo:

1. DAVID JOHN MAYUBE – Waziri.
2. GEOFREY PHILBERT MULOKOZI – Naibu Waziri.
3. REGINA LYMO – Naibu Waziri (VETA).
4. GOTFRIED MWESIGA JOSEPHATI (katibu)

Ifuatayo ni taarifa ya utendaji kazi ya Wizara ya Elimu 2024/2025 ndani ya muhula wa kwanza wa serikali ya wanafunzi. Taarifa hii imeambatana na malengo, mafanikio, chanagamoto na mipango mikakati.

## MALENGO YA WIZARA YA ELIMU MUHULA WA KWANZA

- Kuandaa kampeni kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kuzingatia na kuwa na uelewa mpana katika mambo yote yahusuyo taaluma.
- Kuwa na taratibu za kupokea changamoto kutoka kwa wawakilishi wa madarasa kupitia vikao vya ASAC na njia nyingine Zaidi mfano:
    - Whatsapp group la Wizara na Wanafunzi wote kwa ujumla
- Kuhakikisha Ofisi ya Mitihani inaweza kuwahisha kutoa kwa fraft ya ratiba kwa ajili ya masomo ya GST ili uongozi wa madara waweze kupanga ratiba kwa ajili ya mitihani yao ya mwisho wa muhula hii itasaidia katika kutatua changamoto ya baadhi ya masomo kukosekana kwenye ratiba.
- Namba za mitihani kuweza kutolewa mapema ili kuepusha changamoto ya mwingiliano wa namba hizo kwa wanafunzi Zaidi ya mmoja.
- Kutoa Elimu ya mafunzo ya Vitendo (Industrial practical training) kwa wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza na wengineo pia, ilikuweza kutambua umuhimu wa kutafuta nafasi za field na kuzingatia ujuzi watakaoenda kupata Zaidi katika sehemu hizo.
- Kuhakikisha ratiba za mitihani za End of Semester zinatolewa kwa wakati ili kama kutatokea mabadiliko ya aina yoyote ile yaweze kufanywa kwa wakati.
- Kuwaelimisha wanafunzi waliodailiwa kwa mwaka wa masomo 2024/2025 juu ya taratibu na za mitihani.
- Kuhakikisha wanafunzi wanaomaliza level 6 na level 8 wanaweza kufanya mitihani yao ya supplementary kwa wakati.
- Kuandaa kampeniii inayolenga kuwakumbusha wanafunzi kitaaluma (Elimu na Soateco mpya).

MAFANIKIO:

Kama Wizara ya Elimu tumeweza kufanikiwa katika mambo mbalimbali yanayohusu Elimu na jamii kwa ujumla, mambo hayo ni kama ifuatavyo:

- Tumefanikiwa kuwa na mawasiliano mazuri baina yetu kama Wizara ya Elimu, uongozi wa chuo, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Mheshimiwa Raisi wetu wa SOATECO. 100%.
- Tumefanikiwa kuweza kuhakikisha namba za mitihani zinaweza kutolewa mapema. Kwa 100%.
    - 80% -> Tayari
    - 10% -> Matatizo maalum ya kimtihani
    - 5% -> Ada
    - 5% ->
- Tumefanikiwa kuandaa kampeni ya kitaaluma (Academic proposal) itakayoanza hivi karibuni kwa kaulimbiu ya "Elimu na soateco mpya". Itakayolenga mambo yafuatayo.
    - Industrial practical training (IPT).
    - Sheria za mitihani (Level 6 & 8).
- Tumefanikiwa kutoa ratiba ya End ya Semester kwa haraka ili kuweza kuruhusu wawakilishi wa Madarasa (Cr's) kufanya marekebisho kwa mapema na kuondoa shida ya mitihani kuingiliana.
- Tumefanikiwa kutengeneza uhusiano ulio bora kielimu kati ya chuo chetu cha ATC na vyuo vikubwa hasa upande wa uhandishi kama.
    - DIT.
    - Ardhi.
    - MUST.

# MIPANGO KAZI KATIKA WIZARA YA ELIMU.

- Wizara ina mpango ya kuandaa Makongamano mbalimbali kwa kushirikiana na vyuo vingine kama DIT, Ardhi na MUST kwa ajili ya kukuza taaluma kwa mfano wa mashindano na kusaidia wanafunzi kuweza kupata ufadhili wa kielimu yaani (SCHOLARSHIP).
- Wizara ina mipango ya kuendeleza vikao vya ASAC pamoja na uongozi wa Madarasa kwa muhula huu wa kwanza na wa pili.
- Kuwa na mwendelezo kwa kampeni ya Elimu na Soateco mpya. Ili kuwezesha wanafunzi wa level zote kufaham mambo muhimu hasa
    - Usajili na ulipaji ada
    - Sheria za mitihani
    - IPT
- Wizara ina mpango wa kutimiza moja wapo ya sera ya mhshimiwa Raisi upande wa Elimu.
    - Kuboresha mfumo wa matokeo kuwa na wazi na kumpa mwanafunzi uwezo wa kufahamu mchakato na mchanganuo wa marks zake hadi upatikanaji wa GPA aliyonayo.
    - Maboresho katika sharia na adhabu za kimtihani kama vile re-do.
    - Uanzishwaji wa mfumo rafiki wa ulipaji ada utakao mpa mwanafunzi haki ya msingi ya kushiriki katika mitihani yote bila tatizo lolote kwa kipindi cha ufuatiliaji mchakato wa malipo ya ada yake.
    - Uanzishwaji wa ziara za kimasomo kwa wanafunzi wa idara na levels tofauti katika vyuo vingine nchini vinavyotoa kozi sawa na chuo chetu kama DIT, MUST na Ardhi university. Lengo ni kupata uzoefu mpyam kuongeza ufanisi na mbinu mpya zitakazowezesha kuongeza ufanisi na ujuzi katika kada husika

**HITIMISHO:**

Wizara ya Elimu chini ya serikali ya wanafunzi SOATECO imekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha uzoefu wa Elimu na maendeleo ya wanafunzi wa chuo cha ufundi Arusha.

Hivyo kuna haja kubwa ya kufanya kazi kwa bidii na udanisi wa haili ya juu ilikukabiiana na changamoto zinazojitokeza na kuhakikisha kuwa Wizara inakuwa na thamani bora kwa wanafunzi (Wasoateco) na jamii kwa ujumla.

Imeandaliwa na:

_ _ _ _ _ _ _ _ _ _ _ _ _ _

GOTFRIED MWESIGA JOSEPHATI

Katibu Wizara Ya Elimu

SOATECO